**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**

# HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI OFISI YA RAIS FEDHA NA MIPANGO MHESHIMIWA JAMAL KASSIM ALI (MBM) AKIWASILISHA MWELEKEO WA HALI YA UCHUMI KWA MWAKA 2021 NA MPANGO WA MAENDELEO WA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR KWA MWAKA 2021/2022

**JUNI, 2021**

# HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI OFISI YA RAIS FEDHA NA MIPANGO MHESHIMIWA JAMAL KASSIM ALI (MBM) AKIWASILISHA MWELEKEO WA HALI YA UCHUMI KWA MWAKA 2021 NA MPANGO WA MAENDELEO WA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR KWA MWAKA 2021/2022

## UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** Kwa ruhusa yako napenda kutoa hoja kwamba Baraza lako Tukufu likae kama Kamati ili liweze kujadili na hatimae kuidhinisha Mpango wa Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Hotuba hii ya Mpango wa Maendeleo ninayoiwasilisha leo inaambatana na Kitabu cha Kwanza cha Mapitio ya Hali ya Uchumi ya mwaka 2020 na Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021 pamoja na Kitabu cha Pili cha Mwelekeo

wa Hali ya Uchumi kwa mwaka 2021 na Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2021/2022. Uwasilishaji wa Hotuba hii na taarifa za vitabu hivyo umezingatia Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya mwaka 2050, mwelekeo wa Mpango wa Muda wa Kati wa Maendeleo wa Zanzibar 2021-2025, Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala cha CCM ya mwaka 2020-2025 na makubaliano ya kikanda na ya kimataifa yakiwemo Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Dunia (SDGs) ya mwaka 2015-2030 na Ajenda ya Afrika Tuitakayo ya mwaka 2063.

2. **Mheshimiwa Spika**, Shukurani za dhati ziende kwa Mola wa ulimwengu Muumba wa vyote vilivyomo mbinguni na ardhini kwa kutupa uhai na uzima na uwezo wa kutekeleza majukumu yetu kwa ufanisi hadi muda huu. Ni yeye tu anayestahiki kushukuriwa na viumbe vyote kwa neema anayoendelea kutupa ya uhai na fikra njema za kuendeleza Taifa letu na kuwatumikia

wananchi kwa manufaa yaliyo bora. Tunawaombea shifaa kwa Mwenyezi Mungu waliopatwa na maradhi mbali mbali pamoja na waliopata misukosuko ya ajali, wapate nafuu na waweze kurudi katika hali zao na kuendelea na kazi za kujenga nchi yetu.

3. **Mheshimiwa Spika,** napenda kuwashukuru wananchi wa Zanzibar kwa kufanikisha uchaguzi wa mwaka 2020 kwa amani na utulivu na kupelekea CCM kupata ushindi wa kishindo wa nafasi ya urais pamoja na wawakilishi na wabunge kupitia majimbo mbali mbali Unguja na Pemba. Pongezi na Shukurani za kipekee zimwendee Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kushika usukani wa Awamu ya Nane na kuiongoza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yenye muundo wa Umoja wa Kitaifa kwa umahiri mkubwa. Uongozi wako una dhamira ya dhati ya kuendeleza

hali ya amani na utulivu iliyopo nchini pamoja na kuinua uchumi wa Zanzibar, mkazo ukiwekwa katika kutumia fursa za ***Uchumi wa Buluu***. Dhana hii inaenda sambamba na uendelezaji wa utalii, usimamizi wa uchimbaji wa mafuta na gesi, uimarishaji wa miundombinu, uimarishaji wa sekta binafsi, kupambana na udhalilishaji, rushwa na ubadhirifu, uhifadhi wa mazingira, uwezeshaji wa wananchi pamoja na masuala ya usawa wa kijinsia. Aidha, nimpongeze Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Mama yetu Samia Suluhu Hassan, Rais wa Awamu ya Sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyeshika wadhifa huo baada ya kifo cha Rais wetu Mheshimiwa John Pombe Magufuli. Tunamuomba Mola ampe wepesi wa kuweza kutekeleza majukumu yake na kumuwezesha kulilinda Taifa la Tanzania dhidi ya wasiyoitakia mema nchi yetu. Kwa hakika mama Samia ameweka historia nzuri barani Afrika kuwa mwanamke wa kwanza kwa Afrika ya

Mashariki kushika nafasi ya urais. Hongera mama Samia! Vilevile nitumie nafasi hii kumpongeza Dr. Philip Isidori Mpango kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

4. **Mheshimiwa Spika,** Napenda niwapongeze Makamu wa Kwanza wa Rais Mheshimiwa Othman Masoud Othman na Makamu wa Pili wa Rais Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla, kwa kuteuliwa kushika nafasi kubwa za uongozi katika nchi yetu. Viongozi hawa kwa kweli wanafanya kazi kubwa ya kumshauri na kusimamia shughuli za Serikali na uratibu wa shughuli za Muungano kwa ufanisi mkubwa. Mungu awawezeshe kutimiza majukumu yao, azidi kuwapa wepesi na ari katika usimamizi na ushauri kwa kiongozi wetu wa Taifa ili wananchi wapate manufaa na maendeleo kutokana na uongozi wao.

5. **Mheshimiwa Spika,** Naomba sasa kukupongeza wewe Mheshimiwa Zubeir

Ali Maulid, Spika wa Baraza la Wawakilishi Pamoja na Mheshimiwa Mgeni Hassan Juma, Naibu Spika wa Baraza la Wawakilishi kwa kuchaguliwa tena kushika nafasi hizo. Hii inaonesha imani kubwa kwa wajumbe namna mnavyosimamia na kuviendesha vyema vikao vya Baraza letu kwa ufanisi mkubwa. Tunamuomba Mwenyezi Mungu awazidishie hekima, busara na uweledi katika utendaji wa kazi zenu za kila siku. Pongezi pia nazitoa kwa Mheshimiwa Mwanaasha Khamis Juma kwa kuendelea na wadhifa wako wa Mwenyekiti wa Baraza la Wawakilishi pamoja na Mheshimiwa Shaaban Ali Othman kwa kuchaguliwa kushika nafasi ya Mwenyekiti katika Baraza hilo. Namshukuru sana Mheshimiwa Miraji Khamis Mussa (Kwaza), aliyekuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti ya Baraza la Wawakilishi na wajumbe wake wote. Ushirikiano wa viongozi hawa wote unaleta mafanikio katika upangaji na utekelezaji wa mipango yetu ambayo ni nguzo muhimu kwangu na

kwa Baraza letu hili. Kwa heshima ya pekee, nawapongeza wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi kwa kupata ridhaa za wananchi kutoka majimboni mwao. Hakika tumeaminiwa nasi hatuna budi kuonyesha shukurani zetu kwa wananchi kwa kuwaletea maendeleo.

6. **Mheshimiwa Spika,** Watanzania bado tunakumbuka vifo vya wapendwa viongozi wetu wa Kitaifa, Dkt. Benjamin William Mkapa, aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tatu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Halikadhalika, mnamo tarehe 17 Machi, 2021 msiba mkubwa uliikumba Tanzania baada ya kuondokewa na Rais wetu mpendwa aliyekuwa madarakani, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. Aidha, Wazanzibari tulimpoteza aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar Maalim Seif Sharif Hamad, kiongozi aliyepigania umoja wa Wazanzibari na kuhimiza mashirikiano. Tunawaombea kwa

Mwenyezi Mungu awarehemu na awape makaazi mema.

7. **Mheshimiwa Spika,** Kwa nafasi hii pia naomba nitoe pole kwa Uongozi wa Chama cha ACT–Wazalendo kufuatia vifo vya wawakilishi wawili wa wananchi vilivyotokea katika muda tofauti, Nd. Abubakar Khamis, aliyekuwa mwakilishi wa Jimbo la Pandani na Nd. Khatib Said Haji aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Konde Pemba. Mwenyezi Mungu awalaze mahala pema peponi Amin. Dua hii pia tunawaombea wazee, ndugu na jamaa zetu wote waliotangulia mbele ya haki tukijua kuwa kazi ya Mola haina makosa. Na sisi tuliobakia tunaomba utuzidishie afya njema, uvumilivu na baraka katika majukumu ya kazi zetu za kila siku. Mijadala hii inayoendelea katika Baraza letu tukufu tunaomba iwe na baraka, upendo uvumilivu na mshikamano baina yetu ili kuleta tija kwa nchi na wananchi kwa ujumla. Kwa nafasi hii pia napenda kumpongeza Prof. Omar

Fakih Hamad kwa kuchaguliwa kuwa mwakilishi wa Jimbo la Pandani na kushika nafasi ya Marehemu Abubakar. Wananchi wa jimbo la Pandani wana matumaini makubwa juu yako na tunaamini utawawakilisha vyema katika kuwatatulia changamoto zao mbali mbali.

8. **Mheshimiwa Spika**, Nachukua fursa hii kumshukuru tena Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kuniamini na kuniteua kuiongoza Ofisi ya Rais Fedha na Mipango. Naelewa jukumu nililonalo ni kubwa lakini ushirikiano anaonipatia, unanisaidia sana kutekeleza majukumu yangu kwa ufanisi mkubwa. Naomba ushirikiano huo uzidi kuendelea. Aidha, napenda kuwashukuru wafanyakazi wote pamoja na familia yangu kwa kuwa na mimi muda wote na kuniunga mkono na kunisaidia ipasavyo katika kufanikisha majukumu yangu ya kazi. Naamini kwa juhudi kubwa na maarifa

wanayonipatia nitaweza kutekeleza majukumu yangu kwa uadilifu na ufanisi zaidi na kukidhi kiu ya maendeleo ya wananchi wa Zanzibar.

9. **Mheshimiwa Spika**, wakati Dunia ikiendelea na mbinu mbali mbali za kujenga uchumi wake, janga la Corona lililojitokeza mwishoni mwa mwaka 2019 linarudisha nyuma jitihada hizo. Maelfu ya wananchi kote duniani wamepoteza maisha yao na chumi za nchi mbali mbali kudidimia. Zanzibar na Tanzania kwa ujumla inaendelea na jitihada za kufuatilia kwa makini ili kupunguza madhara ya maradhi hayo kwa nchi yetu. Mola awape nuru wataalamu wa mataifa mbali mbali kuwawezesha kupata maarifa zaidi ya kuweza kutokomeza maradhi hayo thakili.

10. **Mheshimiwa Spika,** naomba nimpongeze Rais mstaafu Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kudumisha utulivu na amani na kumkabidhi kijiti cha kuongoza nchi

hii Dkt. Hussein Ali Mwinyi. Bila ya shaka, ushirikiano wa marais wastaafu utaendelea kwa maslahi ya Zanzibar na watu wake. Ni wazi kuwa miradi na shughuli zilizoachwa na Dkt. Shein zitaendelezwa na kutunzwa ili tuwe na maendeleo endelevu.

11. **Mheshimiwa Spika**, Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2050 imeshazinduliwa yenye lengo la kuifanya Zanzibar iwe nchi yenye uchumi wa kati kiwango cha juu. Dira hiyo ya miaka 30 utekelezaji wake umepangwa kwa vipindi vitatu vya miaka 10 yenye mwelekeo wa kufanya mageuzi ya kiuchumi na kijamii. Mkazo mkubwa umewekwa kuzifanyia kazi ipasavyo sekta za Uchumi wa Buluu, Mafuta na Gesi na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano ili ziweze kuchangia harakati za ukuzaji uchumi na uimarishaji wa ustawi wa jamii. Aidha, Sekta nyenginezo za ukuzaji uchumi za kilimo, utalii na viwanda na sekta za kijamii za elimu, afya na maji nazo zimepewa msukumo ili kurahisisha

utekelezaji wa sekta nyengine. Kwa muktadha huo, Serikali ya Awamu ya Nane inayoongozwa na Dkt. Hussein Ali Mwinyi, inaanza utekelezaji kwa miaka 10 ya mwanzo ili kuleta maendeleo kwa Wazanzibari wote. Utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2050 utatafsiriwa kwa kuandaa mipango ya muda wa kati ili kuweka misingi imara ya utekelezaji kwa wadau wote.

12. **Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo, naomba kuwasilisha muhutasari wa Mapitio ya Hali ya Uchumi kwa mwaka 2020 na Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa kipindi cha miezi tisa Julai 2020 hadi Machi 2021 pamoja na Mwelekeo wa Hali ya Uchumi kwa mwaka 2021 na Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2021/2022.

## MAPITIO YA HALI YA UCHUMI KWA MWAKA 2020

## Mwenendo wa Uchumi

### *Hali ya Uchumi Duniani*

13. **Mheshimiwa Spika,** Tokea mwishoni mwa mwaka 2019, dunia ilikumbwa na janga la maradhi ya Corona ambalo kwa kiasi kikubwa limeathiri shughuli za kiuchumi na kijamii duniani. Kutokana na hali hiyo, kasi ya ukuaji wa uchumi wa dunia imepungua kwa wastani wa asilimia -3.3 mwaka 2020 ikilinganishwa na asilimia 2.9 mwaka 2019. Hali ya uchumi duniani huathiriwa na mwenendo tofauti katika ukuaji wake kwa Nchi Zilizoendelea, Nchi Zinazoendelea na zile Nchi Zinazoibukia Kiuchumi. Ukuaji wa uchumi kwa nchi hizo ni kama ifuatavyo:

    i. Kasi ya ukuaji wa uchumi kwa Nchi Zilizoendelea imeshuka na kufikia wastani wa asilimia -4.7 kwa mwaka 2020 ikilinganishwa na asilimia 1.7 kwa mwaka 2019;

    ii. Uchumi wa Nchi Zinazoendelea na Nchi Zinazoibukia kiuchumi, kasi ya ukuaji wa uchumi imeshuka na kufikia

wastani wa asilimia -2.2 mwaka 2020, ikilinganishwa na ukuaji wa wastani wa asilimia 3.7 mwaka 2019;

iii. Kasi ya ukuaji wa uchumi wa Afrika imefikia wastani wa asilimia -2.1 mwaka 2020 kutoka ukuaji wa wastani wa asilimia 3.3 mwaka 2019;

iv. Kasi ya ukuaji wa uchumi kwa nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara, imefikia wastani wa asilimia -2.6 kwa mwaka 2020 kutoka wastani wa ukuaji wa asilimia 3.0 mwaka 2019;

v. Kasi ya ukuaji wa uchumi kwa nchi za Afrika Mashariki ilifikia wastani wa asilimia 1.4 mwaka 2020 kutoka wastani wa asilimia 6.6 mwaka 2019.

## Mfumko wa Bei Duniani

14. **Mheshimiwa Spika,** Kasi ya mfumko wa bei duniani kwa mwaka 2020 imeshuka na kufikia wastani wa asilimia 3.2 kutoka wastani wa asilimia 3.6 mwaka 2019. Hii imetokana na kushuka kwa bei kwa bidhaa zenye mahitaji makubwa katika kipindi cha

maradhi ya Corona. Mfumko wa bei duniani ulikuwa kama ifuatavyo:

i. Nchi Zilizoendelea kasi ya mfumko wa bei imefikia asilimia 1.6 mwaka 2020 kutoka asilimia 1.8 mwaka 2019;
ii. Nchi Zinazoendelea na Zinazoibukia kiuchumi kasi ya mfumko wa bei imepanda kidogo na kufikia wastani wa asilimia 4.9 mwaka 2020 kutoka wastani wa asilimia 4.7 mwaka 2019;
iii. Kasi ya mfumko wa bei wa nchi za Afrika imepanda kufikia wastani wa asilimia 10.4 mwaka 2020 kutoka wastani wa asilimia 9.8 mwaka 2019;
iv. Kasi ya mfumko wa bei kwa nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara imeongezeka kufikia wastani wa asilimia 3.2 mwaka 2020 kutoka wastani wa asilimia 2.7 mwaka 2019;
v. Kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kasi ya mfumko wa bei imeongezeka na kufikia wastani wa asilimia 5.9 mwaka 2020 kutoka wastani wa asilimia 2.7 mwaka 2019.

## Ukuaji wa Uchumi wa Zanzibar

15. **Mheshimiwa Spika,** Wakati uchumi wa dunia ukipungua kwa wastani wa asilimia 3.3 na uchumi wa Jumuia ya Afrika Mashariki ukikua kwa kasi ya wastani wa asilimia 1.4 mwaka 2020, uchumi wa Zanzibar umeendelea kuwa imara na kukua kufikia wastani wa asilimia 1.3 mwaka 2020 kutoka wastani wa asilimia 7.0 mwaka 2019. Ukuaji huo ni wa kuridhisha ikilinganishwa na nchi nyengine duniani.

Miongoni mwa sababu za ukuaji huo wa uchumi ni pamoja na:

i. Kuongezeka kwa upatikanaji wa ajira katika sekta za umma na binafsi kufikia 67,095 mwaka 2020 kutoka ajira 62,804 mwaka 2019;
ii. Kongezeka kwa uzalishaji wa kuku kutoka 120,288 mwaka 2019 kufikia 709,930 kwa mwaka 2020;
iii. Kuongezeka kwa Usafirishaji wa bidhaa katika sekta ya biashara kufikia

TZS 65,661.0 milioni mwaka 2020 kutoka TZS 48,573.3 milioni mwaka 2019;

iv. Kuendelea kuwepo kwa hali ya amani na utulivu nchini.

**Pato Halisi la Taifa**

16. **Mheshimiwa Spika,** Pato Halisi la Taifa limeendelea kuwa zuri ambapo kwa mwaka 2020 lilifikia thamani ya TZS 3,116 bilioni ikilinganishwa na thamani ya TZS 3,078 bilioni mwaka 2019.

**Pato la Mwananchi**

17. **Mheshimiwa Spika,** Pato la Mtu Binafsi kwa mwaka 2020 limepungua na kufikia TZS 2,526,000 sawa na Dola za Kimarekani 1,099 ikilinganishwa na TZS 2,551,000 sawa na Dola za kimarekani 1,114 mwaka 2019. Kupungua huko kwa Pato la Mtu Binafsi kunatokana na ukuaji mdogo wa uchumi wa wastani wa asilimia

1.3 ikilinganishwa na kasi ya ongezeko la Idadi ya Watu ya wastani wa asilimia 2.8.

**Mfumko wa Bei**

18. **Mheshimiwa Spika,** kasi ya mfumko wa bei katika mwaka 2020 imepanda na kufikia wastani wa asilimia 3.4 kutoka wastani wa asilimia 2.7 mwaka 2019. Kupanda kwa kasi ya mfumko wa bei kumechangiwa na kupanda kwa mfumko wa bei za bidhaa za chakula ambapo kasi yake imefikia wastani wa asilimia 5.8 mwaka 2020 kutoka wastani wa asilimia 2.8 mwaka 2019. Hii imetokana na kupungua kwa uzalishaji wa bidhaa zinazozalishwa ndani na kupanda kwa bei za bidhaa muhimu za chakula kutoka nje ya nchi na kutumika hapa nchini kama vile mchele na mafuta ya kupikia.

Kwa upande wa bidhaa zisizo za chakula kasi ya mfumko wa bei imeshuka na kufikia wastani wa asilimia 1.7 mwaka 2020 kutoka wastani wa asilimia 2.6 mwaka 2019. Hii imetokana na kupungua kwa bei za bidhaa za nishati ya mafuta

duniani na utulivu wa thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi ya dola ya kimarekani.

19. **Mheshimiwa Spika,** Miongoni mwa hatua zilizochukuliwa na Serikali katika kudhibiti mfumko wa bei ni pamoja na:

i. Kuendelea kushajiisha wawekezaji wazalendo wa nje na ndani kuwekeza katika sekta ya viwanda vidogo vidogo na vya kati nchini;

ii. Benki Kuu ya Tanzania (BOT) kuendelea kudhibiti mwenendo wa sarafu ya Tanzania dhidi ya sarafu nyengine pamoja na kuimarisha Sera za kifedha;

iii. Kuendelea kushajiisha wakulima kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula na mboga;

iv. Kuendelea kufuatilia mwenendo wa bei kwa wafanyabiashara wa bidhaa za chakula na nishati ya mafuta.

**Ukuaji na Mchango wa Sekta Katika Pato la Taifa**

***Ukuaji wa Sekta katika Pato la Taifa***

20. **Mheshimiwa Spika**, Sekta ya Huduma inajumuisha sekta ndogo za Malazi na huduma za chakula, Sanaa, burdani na ubunifu, Afya, Elimu, Mawasiliano na kadhalika. Ukuaji wa sekta ya huduma katika Pato la Taifa kwa mwaka 2020 ulifikia wastani wa chini ya asilimia 1.0 ikilinganishwa na ukuaji wa wastani wa asilimia 8.7 mwaka 2019. Kupungua kwa ukuaji wa Sekta hii kumesababishwa zaidi kwa kupungua kwa sekta ndogo ya Malazi na huduma za chakula kutoka asilimia 11.5 mwaka 2019 na kufikia asilimia -12.7 mwaka 2020.

21. **Mheshimiwa Spika,** Sekta ya Viwanda inajumuisha sekta ndogo ya uzalishaji viwandani, ujenzi, uchimbaji mawe na mchanga na kadhalika. Kwa mwaka 2020, Sekta hii imekua kwa kasi ndogo ya asilimia 5.2 ikilinganishwa na asilimia 10.6 mwaka 2019. Kupungua kwa ukuaji katika Sekta hii kumesababishwa na kupungua kwa uzalishaji kwa Sekta ndogo ya uzalishaji viwandani kutoka wastani wa asilimia 20.5 mwaka 2019 na kufikia wastani wa asilimia 6.5

mwaka 2020. Vile vile, kushuka kwa ukuaji wa Sekta ndogo ya huduma za usambazaji maji safi na uchukuzi wa maji machafu na kufikia wastani wa asilimia 2 mwaka 2020 kutoka wastani wa asilimia 12.6 mwaka 2019.

22. **Mheshimiwa Spika,** Sekta ya Kilimo inajumuisha sekta ndogo za mazao, uvuvi, mifugo na misitu. Katika mwaka 2020 ukuaji wa sekta hii katika Pato la Taifa umefikia wastani wa asilimia 3.3 kutoka ukuaji wa wastani wa asilimia 2.6 mwaka 2019. Ukuaji katika sekta ya kilimo umetokana na kuongezeka kwa uzalishaji katika sekta ndogo ya mazao kutoka wastani wa asilimia -5.8 mwaka 2019 na kufikia wastani wa asilimia 1.3 mwaka 2020. Aidha sekta ndogo ya uvuvi uzalishaji wake umeongezeka na kufikia wastani wa asilimia 3.5 mwaka 2020 kutoka wastani wa asilimia 3.3 mwaka 2019.

***Mchango wa Sekta katika Pato la Taifa***

23. **Mheshimiwa Spika,** Sekta ya Huduma imeendelea kuwa na mchango mkubwa zaidi katika Pato la Taifa kwa kuchangia asilimia 47.8

mwaka 2020, kutoka kiwango cha asilimia 50.7 mwaka 2019. Sekta ya Kilimo imekuwa ya pili kwa kuendelea kuchangia wastani wa asilimia 22.8 mwaka 2020 ikilinganishwa na mchango wa asilimia 21.2 mwaka 2019 na Sekta ya Viwanda imechangia kwa wastani wa asilimia 19.6 mwaka 2020 ikilinganishwa na mchango wa wastani wa asilimia 18.1 mwaka 2019.

**Sekta ya Utalii**

24.**Mheshimiwa Spika,** idadi ya watalii na wageni walioingia nchini kupitia kiwanja cha ndege na bandari ya Zanzibar imepungua kwa asilimia 51.6 kufikia watalii 260,644 mwaka 2020 kutoka watalii 538,264 mwaka 2019. Nchi ambazo ziliongoza kwa kuleta watalii wengi mwaka 2020 ni Urusi asilimia 16.7 ikifuatiwa na Ufaransa asilimia 8.5 ya watalii wote waliofika nchini.

**Sekta ya Nje**

25.**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha mwaka 2020 nakisi ya biashara imeongezeka na kufikia

thamani ya TZS 781.8 bilioni ikilinganishwa na thamani ya TZS 706.7 bilioni sawa na ongezeko la asilimia 9.6.

Thamani ya usafirishaji wa bidhaa nje ya nchi imeongezeka kutoka bidhaa zenye thamani ya TZS 48.6 bilioni mwaka 2019 hadi TZS 65.7 bilioni mwaka 2020 sawa na ongezeko la asilimia 35.1. Ongezeko hilo limetokana na kuongezeka kwa usafirishaji wa zao la karafuu kutoka tani 1,744.90 zenye thamani ya TZS 19.8 bilioni mwaka 2019 hadi tani 3,506.8 zenye thamani ya TZS 38.37 bilioni mwaka 2020 na kuongezeka kwa usafirishaji wa zao la mwani kutoka tani 11,203.70 zenye thamani ya TZS 10.3 bilioni mwaka 2019 na kufikia tani 11,382.6 zenye thamani ya TZS 11.7 bilioni mwaka 2020.

Aidha, uagiziaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi umeongezeka na kufikia TZS 847.4 bilioni mwaka 2020 ikilinganishwa na thamani ya TZS 755.3 bilioni mwaka 2019 sawa na ongezeko la asilimia 12.2.

## UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO KWA KIPINDI CHA JULAI 2020 HADI MACHI 2021

26. **Mheshimiwa Spika,** Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2020/2021 unamaanisha ukamilishaji wa utekelezaji wa Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Zanzibar Awamu ya Tatu (MKUZA III) ambao unakamilika rasmi Juni 2021. MKUZA III umeendeleza mageuzi ya kiuchumi na kijamii na kupunguza umasikini kwa (i) Kuwezesha ukuaji wa uchumi jumuishi na endelevu; (ii) Kukuza uwezo wa watu; (iii) Kutoa huduma bora kwa wote; (iv) Kuweka mazingira endelevu na uhimili wa mabadiliko ya tabianchi; na (v) Kushikamana na misingi ya utawala bora.

27. **Mheshimiwa Spika,** Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2020/2021 ulilenga kutekeleza jumla ya programu 24 na miradi 53. Jumla ya TZS 609.9 bilioni zilipangwa kutumika kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa Mpango

huo ikiwa ni ongezeko la TZS 32.9 bilioni sawa na asilimia 5.7 ikilinganishwa na bajeti ya Maendeleo ya mwaka 2019/20 ya TZS 577.0 bilioni. Kati ya fedha hizo, Serikali ilipanga kutumia TZS 197.3 bilioni sawa na asilimia 32.3 ya bajeti ya maendeleo kutoka fedha za ndani. Jumla ya TZS 412.7 bilioni sawa na asilimia 67.6 zilipangwa kutolewa na Washirika wa Maendeleo ikiwa TZS 72.2 bilioni ni ruzuku na TZS 340.5 bilioni ni mkopo.

28. **Mheshimiwa Spika,** Hadi Machi 2021, jumla ya TZS 166.3 bilioni sawa na asilimia 27 ya lengo la TZS 609.9 bilioni zilitumika katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo. Kati ya fedha hizo, TZS 49.2 bilioni sawa na asilimia 25 ya lengo la TZS 197.3 bilioni zilitoka Serikalini na TZS 117.1 bilioni sawa na asilimia 28 ya lengo la 412.7 bilioni zilitoka kwa Washirika wa Maendeleo.

***Utekelezaji wa Maeneo ya Vipaumbele kwa Kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021***

29.**Mheshimiwa Spika,** Ili kuhakikisha utekelezaji wa MKUZA III unafanyika kwa ufanisi, miradi mbalimbali ilipewa kipaumbele kufikia malengo ya maendeleo na kukuza uchumi na kuimarisha ustawi wa wananchi. Utekelezaji wa Programu na miradi 13 iliyopewa kipaumbele katika Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2020/2021 ni kama ifuatavyo:

(i) ***Ukamilishaji wa jengo la tatu la abiria la Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume (Terminal III):*** Ujenzi wa jengo hilo umefikia asilimia 99. Shughuli zinazoendelea ni uwekaji wa alama katika eneo la kuegesha, kurukia na kutulia ndege, uwekaji wa mifumo ya baridi, uzimaji moto, mifumo ya TEHAMA ya kuongozea ndege na kufanya majaribio ya mifumo hiyo pamoja na umeme;

(ii) ***Ujenzi wa Hospitali mpya ya Rufaa ya Binguni***; Kazi ya ujenzi wa hospitali hiyo imeanza kwa shughuli za usafishaji katika eneo la ujenzi wa jengo la Wodi la huduma za dharura (emergency ward). Katika Awamu ya kwanza, jumla ya majengo matano yanatarajiwa kujengwa yakiwemo jengo la (i) huduma za dharura, (ii) utawala, (iii) upasuaji na uchunguzi (iv) mama na mtoto na (v) nyumba ya wafanyakazi.

(iii) ***Ujenzi wa Hospitali ya Wete kuwa na hadhi ya Mkoa***: Utambuzi wa eneo lote la hospitali lenye ukubwa wa mita za mraba 35,219 umefanyika, ambapo mazungumzo na taasisi nyengine ambazo zimejenga katika eneo hilo yamefanyika.

(iv) ***Kukamilisha ujenzi wa Mahakama Kuu Tunguu***: Ujenzi huu unaendelea kwa hatua za ukamilishaji ikiwemo kuweka sawa mifumo ya umeme na kadhalika. Kwa ujumla, ujenzi umefikia asilimia 80.

(v) ***Kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji maji katika mabonde ya Chaani, Kinyasini, Kibokwa, Kilombero na Cheju kwa Unguja na Makwararani na Mlemele kwa Pemba yenye ukubwa wa hekari 1,524:*** Ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji maji kwa mabonde hayo unaendelea, ambapo kwa ujumla ujenzi umefikia asilimia 40.5.

(vi) ***Ujenzi wa Bandari ya Mpigaduri***; Kazi za upembuzi yakinifu na utafiti wa kijiolojia zimekamilika.

(vii) ***Kuendeleza ujenzi wa mji wa kisasa Kwahani***; Ujenzi wa majengo matano ya awamu ya kwanza umekamilika. Wananchi 51 wamekabidhiwa funguo zao na wameshahamia.

(viii) ***Kuimarisha sekta ya mafuta na gesi kwa kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya matangi ya kuhifadhia mafuta katika eneo la Bandari ya Mangapwani***: Maandalizi ya ujenzi wa Bandari ya Mangapwani yameanza. Ulipaji wa fidia wa wakaazi waliohamishwa eneo la Dundua umekamilika kwa wananchi wanaohusika kukabidhiwa nyumba zao. Aidha, Serikali imeanza kuandaa mpango mkuu (master plan) wa ujenzi.

(ix) ***Kuimarisha ulinzi na usalama***: Serikali imeendelea kuimarisha ulinzi na usalama wa nchi kwa kuendelea na awamu ya pili ya uwekaji wa kamera mpya katika maeneo mbalimbali. Ufungaji wa kamera katika miji ya Chakechake, Mkoani na Wete kwa Pemba umekamilika na uwekaji wa kamera za ulinzi na usalama (CCTV) katika maeneo ya Kiembe Samaki –Baraza la Wawakilishi na Mazizini – Buyu unaendelea. Matayarisho ya uwekaji wa miundombinu ya uwekaji wa CCTV camera katika maeneo ya Amani – Mboriborini na Shaurimoyo, Amani – Mwera, Mtoni – Bububu na Mombasa - Fumba yanaendelea.

(x) ***Ujenzi wa barabara ya Chake Chake – Wete:*** Ripoti ya upembuzi yakinifu pamoja na tathmini ya

nyumba na mali zitakazo athirika na ujenzi wa barabara hiyo imeshaandaliwa na kuwasilishwa; na

(xi) ***Ujenzi wa kituo cha maonesho ya biashara na mikutano ya kimataifa (Convention Centre) kwa mfumo wa mashirikiano ya sekta ya umma na sekta binafsi***: Utekelezaji wa mradi huu umeanza ambapo kazi ya Tathmini ya kimazingira katika eneo la mradi imekamilika. Aidha, mkutano wa wadau mbali mbali ambao watahusika katika mradi umefanyika wakiwemo wakaazi wa Nyamanzi pamoja na Taasisi zinazohusika na masuala ya utalii kujadiliana kuhusu mradi huo.

30.**Mheshimiwa Spika,** Utekelezaji wa miradi mengine ya maendeleo iliyotekelezwa kwa kipindi cha mwaka 2020/2021 inaonekana katika kitabu cha kwanza cha Mapitio ya Hali

ya Uchumi 2020 na Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2020/21.

## MWELEKEO WA HALI YA UCHUMI KWA MWAKA 2021

### Mwelekeo wa Uchumi wa Dunia

31. **Mheshimiwa Spika,** Kutokana na kuendelea na janga la ugonjwa wa Corona kumepelekea Uchumi wa dunia kuzorota na kuripotiwa athari kubwa katika sekta zote duniani ikiwemo Utalii, Usafiri wa anga, usafirishaji na biashara, sekta za kifedha na sekta nyengine za kijamii. Hivyo, kwa mwaka 2021 matarajio ya kasi ya ukuaji wa Uchumi duniani ni kufikia wastani wa asilimia 6.0. Matarajio ya ukuaji wa uchumi kwa maeneo mengine ni kama ifuatavyo:

    i. Kasi ya ukuaji wa Uchumi kwa Nchi Zilizoendelea inatarajiwa kupanda na kufikia wastani wa asilimia 5.1 mwaka 2021;
    ii. Nchi Zinazoendelea na Zinazoibukia Kiuchumi, kasi ya ukuaji wa Uchumi

inatarajiwa kupanda na kufikia wastani wa asilimia 6.7 mwaka 2021;

iii. Nchi Zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara kasi ya ukuaji inatarajiwa kufikia wastani wa asilimia 3.7 kwa mwaka 2021.

**Mwelekeo wa Uchumi wa Zanzibar 2021**

32.**Mheshimiwa Spika,** Mwelekeo wa hali ya uchumi wa Zanzibar kwa mwaka 2021 unategemewa kuimarika na kuinua hali za wananchi. Kwa mwaka 2021, Pato la Taifa linatarajiwa kukua kwa kasi ya wastani wa baina ya asilimia 5.0 hadi asilimia 7.0 kutokana na matarajio ya kuongezeka kwa shughuli mbali mbali za maendeleo ikiwemo kuanza miradi mikubwa ya maendeleo, kuwa na sera nzuri na jumuishi za uwekezaji pamoja na kuweka mifumo imara ya ukusanyaji kodi. Hata hivyo, kutokana na kuendelea kuwepo kwa janga la ugonjwa wa COVID 19 duniani, uchumi wa Zanzibar unatarajiwa kukua kwa kasi ya chini ya asilimia 5.2. Hii ni kutokana na kuyumba kwa

sekta za uchumi ikiwemo utalii, biashara na uwekezaji.

**Shabaha na Malengo ya Uchumi kwa Mwaka 2021-2023**

33. **Mheshimiwa Spika,** Shabaha na malengo ya uchumi kwa kipindi cha miaka mitatu yanategemewa kuwa kama ifuatayo;

i. Kasi ya ukuaji wa Pato la Taifa inategemewa kukua baina ya asilimia 5.0 hadi asilimia 7.0;
ii. Kuendelea kudhibiti kasi ya mfumko wa bei kuwa katika wastani wa chini ya asilimia tano (5);
iii. Kuendelea kuwepo kwa amani na utulivu duniani;

34. **Mheshimiwa Spika,** Shabaha nyengine za msingi ni pamoja na:-

a. Uwajibikaji katika kazi;
b. Kuendelea kuwajengea uwezo wafanyakazi;
c. Kuimarisha utawala bora;

d. Kutengeneza mifumo bora ya usimamizi wa makusanyo ya kodi;
e. Kuendelea kuwa na uhusiano mzuri na nchi Jirani;
f. Kupanda kwa thamani ya bidhaa za kusafirisha duniani ikiwemo karafuu na mwani;
g. Kuongezeka kwa uzalishaji na uwekezaji katika kanda ya Afrika Mashariki;
h. Kushuka kwa bei za nishati katika soko la dunia;
i. Kuendelea kuweka sera bora na za kiushindani za uwekezaji;
j. Kuondoa ubadhirifu wa Mali ya Umma, Wizi, Rushwa pamoja na Uzembe.

## MWELEKEO WA MPANGO WA MAENDELEO KWA MWAKA 2021/22

35.**Mheshimiwa Spika,** Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo kwa kipindi cha mwaka

2021/2022 utazingatia malengo na mikakati inayotokana na Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2050. Dira hiyo ina lengo la kuifikisha Zanzibar katika Kiwango cha Juu cha Uchumi wa Kati kupitia mihimili mikuu minne ambayo ni **Mageuzi ya Kiuchumi**; **Maendeleo ya Rasilimali Watu na Huduma za Kijamii; Kuimarisha Miundombinu; na Utawala Bora na Uhimili**. Katika kuhakikisha malengo ya dira hiyo yanafikiwa, Serikali imeanza kutafsiri malengo hayo kwa kuandaa mpango ya Maendeleo wa muda wa kati 2021 – 2025 ambapo rasimu ya Mpango huo imekamilika na ipo katika hatua za mwisho kuidhinishwa.

36. **Mheshimiwa Spika,** Mbali na Dira ya Maendeleo ya 2050, Mpango wa Maendeleo 2021/22 umezingatia Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020-2025, Hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi wakati wa ufunguzi wa Baraza la 10 la Wawakilishi, Maelekezo ya Serikali kiujumla pamoja na

ahadi mbali mbali zilizotolewa na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa wananchi wakati wa kampeni ya Uchaguzi na katika ziara za makundi mbali mbali.

## MAPENDEKEZO YA MAENEO YA VIPAUMBELE KWA MWAKA 2021/22

37. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka 2021/22, maeneo ya vipaumbele yanajikita katika kutekeleza mipango mikakati ya nchi inayolenga ukuaji wa haraka ambao utahakikisha maendeleo ya wananchi na ukuaji wa uchumi ulio endelevu pamoja na huduma bora kwa ustawi wa jamii. Kulingana na malengo hayo, maeneo ya kipaumbele na miradi itakayotekelezwa ni kama yafuatayo:

i. ***Kuimarisha maeneo ya uingiaji nchini*:**
Eneo hili linahusisha kuendeleza maeneo mawili makuu:

a. ***Ujenzi wa Bandari ya Mangapwani:*** Kufuatia kukamilika kwa Mpango Mkuu wa Matumizi ya eneo la Bandari ya Mangapwani wenye kujumuisha ujenzi wa bandari ya mizigo; mafuta na gesi; chelezo; ghala na nyumba za makaazi; Serikali inaendelea kufanya mazungumzo na wawekezaji mbali mbali kwa njia ya ubia au binafsi ili kuendeleza eneo hilo kwa mujibu wa mpango mkuu uliowekwa;

b. ***Ujenzi wa uwanja wa ndege wa Pemba:*** Serikali inaendelea na juhudi za kutafuta rasilimali fedha kwa ajili ya ujenzi wa uwanja wa ndege wa Pemba kufuatia kukamilika kwa upembuzi yakinifu;

ii. ***Kuimarisha uchumi wa buluu***

38. **Mheshimiwa Spika,** Katika kuinua hali za wananchi na kuitumia vyema rasilimali ya bahari, Serikali inakusudia kununua meli nne za uvuvi katika kipindi cha miaka mitano ijayo ambapo kwa mwaka 2021/22, ununuzi

wa meli moja utafanyika. Meli hizo zitawezesha kuimarika kwa shughuli za uvuvi wa bahari kuu nchini. Serikali pia itashajiisha uanzishaji wa mashamba ya kufugia samaki kwa wananchi na kutoa taaluma na mbinu bora za ufugaji wa samaki na ukulima wa mwani. Serikali inakamilisha upembuzi yakinifu wa ujenzi wa Bandari ya uvuvi ya Mpigaduri na Mkoani. Juhudi za kutafuta wawekezaji zitafanyika mara baada ya kukamilika kwa upembuzi huo.

iii. ***Kuimarisha Miundombinu***

39.**Mheshimiwa Spika,** Eneo hili litajumuisha ujenzi wa barabara ya Chake Chake – Wete (km 22.1); Kuendelea na uwekaji wa miundombinu ya maji katika visima vya Ras el Khaimah na usambazaji wa maji mijini na vijijini; Kuendelea na juhudi za kuimarisha nishati mbadala sambamba na kushajiisha wawekezaji wa ndani na nje kwenye uzalishaji wa umeme wa jua na gesi. Pamoja na hayo, Serikali inakusudia kutafuta mkopo

kwa ujenzi wa kilomita 200 za barabara kuu na kilomita 200 za barabara za ndani

iv. ***Kuimarisha Sekta Kuu za Uchumi***

40. **Mheshimiwa Spika,** Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi ina dhamira ya kuinua uchumi na kuongeza ajira kwa kuendeleza viwanda vidogo vidogo vya usarifu wa Mwani, chumvi na Samaki. Aidha, Serikali itaendelea na ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji maji ili kuongeza uzalishaji wa mazao, mboga na matunda na kuendelea na utekelezaji wa programu ya ajira kwa vijana. Aidha, Serikali itaanza utekelezaji wa mradi wa Mpango Shirikishi wa Kukuza Uchumi Zanzibar (Boost Inclusive Growth in Zanzibar- Big Z) wenye lengo la kuimarisha huduma za miji kwa kuweka mazingira bora na salama.

v. ***Kuimarisha Huduma za Kijamii***

41. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kuzingatia umuhimu wa afya kwa jamii, Serikali itaendelea na ujenzi wa Hospitali Mpya ya

rufaa na kufundishia Binguni na kuanza ujenzi wa Hospitali ya Wete ili kuwa na hadhi ya hospitali ya Mkoa. Serikali pia inakusudia kukuza miundombinu ya elimu kwa kukamilisha madarasa yaliyoanzishwa kwa nguvu za wananchi na kufanya matengenezo ya majengo ya skuli yaliyochakaa pamoja na kuandaa mitaala mipya ya elimu ya msingi na maandalizi.

*vi.* ***Kuimarisha Ofisi za Serikali***

42.**Mheshimiwa Spika,** Katika kuimarisha mazingira mazuri ya ufanyaji kazi, Serikali itaendeleza ujenzi wa ofisi zake zikiwemo Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango Unguja, Taasisi za Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Ofisi ya Mamlaka ya Uhifadhi wa Mazingira (ZEMA) na Ofisi za Serikali Jijini Dodoma. Aidha, ujenzi wa Mahanga na Ofisi za Idara Maalum za SMZ utaendelea. Serikali pia inakusudia kuanza matayarisho ya mji wa Serikali ambapo taasisi nyingi za Serikali zitajengwa katika mji huo.

vii. ***Kuendeleza Rasilimali Watu na Fedha***

43.**Mheshimiwa Spika,** Eneo hili litahusisha kuendeleza taaluma katika fani mbali mbali ikiwemo mafuta na gesi, uhandisi, huduma za ugani, udaktari na taaluma za sayansi. Aidha, Serikali itaimarisha mifumo ya kidijitali ya utendaji kazi kwa ujumla ikiwemo ukusanyaji mapato, usimamizi wa matumizi, manunuzi na utunzaji wa kumbukumbu za usajili wa mali za umma ili kuimarisha taarifa za Serikali na upatikanaji wa mapato.

***Mashirikiano baina ya Serikali, Sekta Binafsi na wadau mbali mbali***

44.**Mheshimiwa Spika,** Katika kuhakikisha maendeleo ya nchi na wananchi yanapatikana kwa haraka na ushiriki wa pamoja, Serikali itakuwa karibu na tayari kushirikiana na sekta binafsi, taasisi za kifedha, wafanyabiashara, Washirika wa Maendeleo na jumuiya zisizo za Kiserikali na wananchi katika kutekeleza miradi kwa njia mbali mbali ikiwemo

mashirikiano ya sekta za umma na binafsi (PPP) na uwekezaji binafsi. Kwa muktadha huo, Serikali imefanya uchambuzi wa programu na miradi mbali mbali na kuweka utaratibu wa kuiendeleza miradi hiyo kwa njia tofauti kama ifuatavyo:

***(i) Miradi itakayotekelezwa na Serikali na Washirika wa Maendeleo kwa mwaka 2021/22***

Eneo hili linajumuisha program na miradi ambayo itatekelezwa na Serikali pekee au kwa mashirikiano na Washirika wa Maendeleo. Orodha kamili ya program na Miradi hiyo inapatikana katika Kitabu cha Pili cha Mwelekeo wa Hali ya Uchumi 2021 na Mpango wa Maendeleo 2021/22.

***(ii) Miradi itakayotekelezwa kwa Mashirikiano ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP)***

45.**Mheshimiwa Spika,** Katika kuimarisha dhana ya mashirikiano baina ya Serikali na

sekta binafsi inayotiliwa mkazo na Serikali ya Awamu ya Nane, Serikali inashajiisha kuwekeza kwa pamoja katika maeneo mbali mbali yakiwemo:

i. Kuendeleza Kituo cha Biashara na Maonyesho ya Kimataifa Zanzibar (Nyamanzi);
ii. Ujenzi wa masoko na vituo vikuu vya mabasi ya abiria (bus stands) maeneo ya Chuini (Kwanyanya), Jumbi, Mkokotoni, Machomane na Ng'ombeni;
iii. Ujenzi wa Dakhalia za Vyuo Vikuu;
iv. Ujenzi wa vituo vya usarifu na uhifadhi wa bidhaa za Samaki.

### (iii) Miradi inayopendekezwa kutekelezwa na sekta binafsi

46. **Mheshimiwa Spika,** Sekta binafsi ina mchango mkubwa katika kukuza uchumi na maendeleo ya jamii. Pamoja na nyanja nyengine, Serikali inashajiisha uwekezaji kwenye maeneo yafuatayo:

    i. Ujenzi wa nyumba za makaazi za bei nafuu;
    ii. Ujenzi wa viwanja vya michezo na burudani;
    iii. Ujenzi wa viwanda vya kuchakata Samaki, mwani, dagaa na kusarifu matunda na mboga;
    iv. Kuanzisha mashamba ya kufugia samaki na majongoo bahari;
    v. Ujenzi wa viwanda vya dawa.

47. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kuzingatia vipengele vyote hivyo, Mpango wa Maendeleo katika kipindi cha miaka mitatu

ijayo unaelekea katika ujenzi wa uchumi ambao unatarajiwa kukua kwa kasi kubwa na kutekeleza miradi mingi ya kimkakati kwa kutumia nyenzo mbali mbali za kuugharamia mpango huo. Kwa mnasaba huo, Serikali imebuni mbinu muafaka za kugharamia mpango huo kwa kushirikisha wawekezaji wakubwa wa ndani na nje ya nchi, sekta binafsi pamoja na kutumia dhana ya ushirikiano baina ya sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP). Halkadhalika, suala la kuitumia vizuri fursa ya mikopo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo nalo limewekewa mkakati maalum katika kutekeleza mpango huo. Kwa utaratibu huo, mpango huu utahimiza kuitekeleza miradi mikubwa ya kimkakati na kuisimamia ili imalizike katika kipindi kifupi kupitia taratibu nilizozieleza hapo juu, badala ya kugharamiwa kidogo kidogo na Serikali kwa fedha chache ambazo zinapangwa kuitekeleza miradi hiyo kila mwaka na kuchukua muda mrefu kumalizika. Kwa mfano, Ujenzi wa Barabara zote kuu za Unguja na Pemba zinazokadiriwa kuwa

kilomita 200 pamoja na barabara za ndani ambazo nazo zinakadiriwa kufikia kilomita 200, unaweza kutekelezwa kwa mkopo na kujengwa katika kipindi cha miaka mitatu tu na Serikali ikapanga kutumia fedha za ujenzi wa barabara zinazokadiriwa kila mwaka ili kulipia deni la ujenzi wa barabara hizo. Mfano huo huo utatumika kwa miradi mengine kama ya Ujenzi wa Hospitali ya Rufaa na ya kufundishia ya Binguni pamoja na miradi mengine ya kimkakati.

48. **Mheshimiwa Spika,** Utaratibu huu utaiwezesha Zanzibar kukuza uchumi wake kwa haraka zaidi pamoja na kuhakikisha kuwepo kwa ajira za uhakika kwa wataalamu wetu na vijana kwa ujumla.

## RASILIMALI KWA AJILI YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO KWA MWAKA 2021/2022

49.**Mheshimiwa Spika**, Kwa mwaka 2021/22, Mpango wa Maendeleo unalenga kutekeleza jumla ya program 25 na miradi 39 ya maendeleo. Kati ya hizo, program tano na miradi 12 ni mipya. Jumla ya TZS bilioni 882.54 zinatarajiwa kutumika kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa programu na miradi ya maendeleo ikiwa ni ongezeko la TZS bilioni 272.55 sawa na asilimia 44.68 ikilinganishwa na bajeti ya maendeleo ya mwaka 2020/2021 ya TZS bilioni 609.99. Kati ya fedha zilizotengwa, Serikali imepanga kutumia TZS bilioni 606.5 sawa na asilimia 69 ya bajeti ya maendeleo ikiwa ni ongezeko la TZS bilioni 410.16 sawa na asilimia 208.9 ya bajeti ya maendeleo ya mwaka 2020/2021. Jumla ya TZS bilioni 276.04 sawa na asilimia 31 zimepangwa kutoka kwa Washirika wa Maendeleo ikiwa TZS bilioni 72.02 ni ruzuku na TZS bilioni 204.02 ni mkopo. Fedha hizo ni upungufu wa TZS bilioni 136.61 sawa na asilimia 33 ikinganishwa na fedha zilizotengwa kwa mwaka 2020/2021 zenye jumla ya TZS bilioni 412.66.

## HITIMISHO

50. **Mheshimiwa Spika,** Napenda kuchukua fursa hii kuipongeza Kamati ya Bajeti ya Baraza la Wawakilishi chini ya Uongozi wa aliyekuwa Mwenyekiti Mheshimiwa Miraji Khamis Mussa (Kwaza), Mwakilishi wa Jimbo la Chumbuni na Waheshimiwa Wajumbe wote wa Kamati kwa kazi kubwa na nzuri walioifanya pamoja na michango na maarifa waliyotupatia hadi kukamilika kwa hotuba hii. Napenda pia kumpongeza Mwenyekiti mpya wa Kamati ya Bajeti Mheshimiwa Ali Suleiman Ameir (Mrembo) kwa kuteuliwa kuiongoza kamati hiyo. Niahidi kutoa ushirikiano kwake katika kutekeleza majukumu ya Kamati hiyo. Shukurani zangu pia nazitoa kwa Waheshimiwa wajumbe wote wa Baraza kwa maoni na ushauri waliotupatia. Ni hakika, maoni na michango yao imerahisisha uandaaji wa Mpango wa Maendeleo na tunategemea mashirikiano mazuri katika utekelezaji wa mipango yetu kwa faida ya wananchi wote.

51.**Mheshimiwa Spika**, Mwisho, si kwa umuhimu, napenda kuwashukuru watendaji wote wa Tume ya Mipango wakiongozwa na Katibu Mtendaji Ndugu Mwita Mgeni Mwita kwa ushirikiano walionipatia katika maandalizi hadi kukamilika kwa Hotuba hii. Aidha, niwapongeze Dkt. Juma Malik Akil Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Fedha na Mipango, Nd. Khamis Suleiman Mwalim Naibu Katibu Mkuu Fedha na Mipango pamoja na Nd. Rashid Said Rashid Naibu Katibu Mkuu Mifumo kwa kuteuliwa kushika nafasi hizo. Nawatakia kheri katika utekelezaji wao wa majukumu mapya. Shukurani zangu ziwaendee Watendaji wote wa Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kwa kufanya kazi kwa pamoja muda wote. Halikadhalika, natoa shukurani za dhati kwa Makatibu Wakuu wa Wizara za SMZ na Watendaji wao wakiongozwa na Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi Mhandisi Zena Ahmed Said. Mhandisi Zena hongera kwa kuteuliwa kuwa Katibu Mkuu

Kiongozi wa Kwanza mwanamke hapa Zanzibar. Ikiwa ni mara yako ya kwanza kufanya kazi nasi, mchango wako ulioutoa tunauthamini pamoja na ushirikiano mkubwa uliotupatia katika matayarisho ya Hotuba hii. Ni matumaini yetu kuwa mashirikiano haya yataendelea kwa kasi na kuhakikisha utekelezaji wa Dira yetu ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2050 na mipango mengine ya maendeleo inakuwa ya ufanisi ili kufikia malengo yetu tuliyoyakusudia kwa manufaa ya wananchi wote.

52.**Mheshimiwa Spika**, Mpango huu wa Maendeleo unatekelezwa na Serikali pamoja na wadau mbali mbali. Michango na misaada ya kifedha na kiutaalamu inayotolewa na wadau tofauti tunaithamini sana na napenda kutoa shukurani za dhati kwa ushirikiano wanaotupatia unaosaidia kuandaa, kutekeleza na kutathmini, mipango yetu ya Maendeleo. Washirika wetu wa Maendeleo wanajumuisha wananchi, sekta binafsi, jumuiya za kiraia, Mashirika ya Kitaifa, Kimataifa na Nchi

Wahisani. Naomba niwatambue washirika na nchi rafiki zinazoendelea kushirikiana nasi kwa mwaka 2021/22 ni pamoja na ACRA, AfDB, AMREF, BADEA, BASKET FUND, CHINA, CANADA, CIDA, CRDB, COSTECH, DANIDA, DFID, EAC, EDF, EU, EXIM BANK, FAO, FINLAND, GAVI, GEF, GLOBAL FUND, HOPELAND UNIVERSITY, HIPZ, GN, GPE, GOOD NEIGHBOUR, IAEA, INDIA, IFAD, ILO, IMF, JAPAN, JICA, KHALIFA FUND, MFUKO WA MAENDELEO WA UMOJA WA FALME ZA KIARABU (UAE), KOREA, KUWAIT, MALAYSIA, ZANZIBAR MILELE FOUNDATION, NMB, NORWAY, OFID, ORIO - NETHERLAND, OMAN, OPEC, PBZ, PMI, QATAR CHARITY ORGANISATION, SAUDI FUND, SAVE THE CHILDREN, SIDA, SWEDEN, THPS, TfT, UK, UN, UNDP, UNEP, UNFPA, UNESCO, UNICEF, UNIDO, URT, USAID, UN WOMEN, UTURUKI, WORLD BANK, WHO na ZSSF.

53.**Mheshimiwa Spika,** Naomba sasa Baraza lako tukufu lipokee na lijadili Mwelekeo wa Uchumi kwa mwaka 2021 na kuidhinisha Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2021/2022 wa TZS bilioni 882.54.

54.**Mheshimiwa Spika,** Naomba Kutoa Hoja.

**JAMAL KASSIM ALI (MBM),**
**WAZIRI WA NCHI**
**OFISI YA RAIS, FEDHA NA MIPANGO,**
**ZANZIBAR**
**JUNI, 2021**